*Sauti za Wananchi* *Muhtasari Na. 37* *Novemba 2016*





# Hali Halisi

## Maoni ya wananchi juu ya elimu bila malipo ya ada

## 1. Utangulizi

Elimu ni nyenzo maalumu inayotofautisha viwango vya maendeleo kati ya nchi tajiri na zile zenye uchumi unaoendelea kukua[1]. Vile vile, tafiti nyingi zinaonyesha kuwa elimu ndiyo huchochea maendeleo. Duniani kote, elimu huhusishwa na maendeleo ya jamii kupitia uimarishaji wa fursa, stadi mahususi, pamoja na kupanua wigo wa mitandao ya watu[2]. Wakati mwingine elimu hupunguza viwango vya uhalifu, kuongeza ushiriki wa raia na kuleta mshikamano[3].

Kwa kutambua umuhimu wa elimu katika kusukuma gurudumu la maendeleo, serikali ya awamu ya tano imeweka suala la elimu katika nafasi ya juu kwenye orodha yake ya vipaumbele. Na ili kupanua wigo na kuhakikisha elimu inapatikana kwa wote, sambamba na kuboresha elimu ya msingi, serikali imeagiza kuwa elimu itolewe bila malipo ya ada kwa shule za msingi na sekondari. Pamoja na hayo, jumla ya shilingi trilioni 4.77[4] zimetengwa kwa ajili ya sekta ya elimu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ukilinganisha na shilingi trilioni 3.887[5] zilizotengwa mwaka 2015/2016, ikiwa ni ongezeko la asilimia 81.3.

Katika mwaka wa kwanza wa uongozi wa Rais Magufuli, serikali, kupitia ruzuku ambayo hutumwa moja kwa moja mashuleni,

1 Aturupane, H., Savchenko, Y., Shojo, M., Larsen, K. (2014). South Asia human development sector. Sri Lanka: Investment in human capital. Discussion Paper Series No. 69. Washington, DC: World Bank Group. Web

2 OECD (2005). *Teachers matter: Attracting, developing and retaining teachers*. Paris: OECD Publishing. Web

3 Green, A. & Preston, J. (2001).Education and social cohesion: Re-centering the debate. *Peabody Journal of Education*, 76 (4): 247-284.

4 Ministry of Finance and Planning, 2016/17 Budget Speech www.mof.go.tz/mofdocs/msemaji/BUDGET%20SPEECH%20FINAL%202016.pdf

5 Ministry of Finance and Planning, 2015/16 Citizens' Budget http://www.mof.go.tz/mofdocs/budget/Citizens%20Budget/CITIZENS%20BUDGET%202015_2016%20_ENGLISH.pdf

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 |
Bp: uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Sauti za Wananchi

Twaweza ni sisi

imeweka msisitizo katika kuhakikisha kuwa shule zote za serikali zinapata nyenzo muhimu na vifaa muhimu. Kipindi cha nyuma ruzuku hizi zilikuwa zikitumwa kwenye mamlaka za wilaya kabla ya kusambazwa mashuleni. Hata hivyo utafiti wa Twaweza umeonyesha kuwa kati ya shilingi 10,000/ kwa mwanafunzi kwa mwaka zilizokuwa zimepangwa[6], wastani wa shilingi 2,000 tu ndizo zilizokuwa zikifika shuleni. Vilevile serikali imewekeza katika kutatua changamoto za miundombinu kama vile madawati na madarasa. Wakati tukielekea mwaka mmoja wa utendaji wa serikali hii, ni wakati mzuri wa kuangalia mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa katika utoaji wa elimu ya msingi.

Muhtsari huu umebeba maoni ya wananchi kuhusu hali ya elimu nchini Tanzania katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Takwimu za muhtasari huu zinatoka Twaweza kupitia utafiti wa *Sauti za Wananchi. Sauti za Wananchi* ni utafiti unaotumia simu za mikononi wenye uwakilishi wa kitaifa. Matokeo haya yana uwakilishi wa Tanzania bara pekee. Taarifa kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana kupitia www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,806 kutoka kundi la pili la Sauti za Wananchi. Hii ilikuwa ni awamu ya kumi ya simu zilizopigwa kwenye kundi jipya, kati ya tarehe 4 na tarehe 17 Agosti 2016.

Matokeo muhimu:

- Kaya 7 kati ya 10 nchini Tanzania zina watoto ambao wanasoma shule za serikali.
- Mwananchi mmoja kati ya watatu anataja upungufu wa walimu (asilimia 34) na madawati (asilimia 30) kama changamoto kubwa zinazokabili shule za serikali nchini Tanzania.
- Wananchi watano kati ya kumi wanasema ubora wa elimu katika shule za binafsi za msingi na sekondari ni nzuri. Hata hivyo, kati ya wananchi kumi, ni wawili walio na mtazamo kama huo kwa shule za serikali.
- Asilimia 85 ya wananchi wametaja kutokujihusisha kwa wazazi kwenye masuala ya elimu ya watoto wao kama tatizo kuu linaloikabili sekta ya elimu.
- Wazazi 7 kati ya 10 wanao uwezo wa kushughulikia matatizo yasiyo ya kitaaluma yanayowaathiri watoto wao wakiwa shuleni. Hata hivyo, wazazi wengi hawajishughulishi na masuala ya elimu ya watoto wao.
- Zaidi ya wananchi 7 kati ya 10 wanasema wasichana walioacha shule kutokana na ujauzito warudi shuleni baada ya kujifungua.


6 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 2 (Juni 2013). Takwimu zinapatikana: www.twaweza.org/sauti

# 2. Mambo sita muhimu kuhusu maendeleo ya sekta ya elimu nchini Tanzania

## Jambo la 1: Asilimia kubwa ya watoto nchini Tanzania wanasoma shule za serikali

Asilimia 80 ya kaya zilitaja kuwa na mtoto ama watoto wanaosoma shule[7]. Wengi wao (asilimia 90) walisema watoto wao wanasoma shule za serikali.

**Kielelezo 1: Je, mtoto wako anasoma shule ya umma au shule ya binafsi?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Wananchi pia walitoa mitazamo yao juu ya uwezo wa shule za serikali kujiendesha bila ada na bila michango ya wazazi. Asilimia 69 walikubali kuwa shule za serikali zina uwezo wa kutoa mahitaji yote ya wanafunzi (chakula, vifaa vya elimu, maji na ulinzi) na asilimia 73 walisema ni sahihi kwa shule kutoa huduma hizo bila kuwahusisha wazazi[8]."


## Jambo la 2: Wananchi watatu kati ya kumi wanasema upungufu wa walimu na madawati ni changamoto kubwa zinazokabili shule za serikali

Shule za serikali zilitajwa kukabiliwa na changamoto nyingi; kuanzia kwenye upatikanaji wa elimu, upungufu wa walimu, mpaka kwenye uduni wa elimu. Wananchi walipoulizwa kuhusu changamoto kubwa inayozikabili shule za serikali katika kipindi cha "bila ada, na bila michango", aslimia 34 walisema upungufu wa walimu na madawati (asilimia 30) bado ni changamoto kubwa. Idadi ndogo (asilimia 13) ya wananchi walitaja ukosefu wa vyumba vya madarasa.

7 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 10 (Agosti 2016). Takwimu zinapatikana: www.twaweza.org/sauti

8 ibid

**Kielelezo cha 2: Ni changamoto zipi zinazokabili shule za serikali tangu zianze kutoa elimu bure?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Pamoja na changamoto hizo, wananchi walipoulizwa kuhusu ubora wa elimu katika shule za serikali kufuatia tamko la elimu bila malipo ada, asilimia 50 walisema wanaamini ubora wa elimu umeongezeka, asilimia 35 walisema umebaki palepale na asilimia 15 waliamini kuwa umeshuka[9].

**Kielelezo cha 2a: Tuambie maoni yako juu ya ubora wa elimu katika shule za serikali tangu kuanzishwa kwa mpango wa elimu bila malipo ya ada**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

## Jambo la 3: Iwapo wangeambiwa wachague, wananchi 6 kati ya 10 wangewapeleka watoto wao shule za binafsi

Asilimia 90 ya kaya zina watoto wanasoma shule za serikali. Lakini endapo shule za binafsi zingekuwa zinatoa elimu bure, asilimia 60 ya wazazi hao wangewahamisha.

9 ibid

**Kielelezo cha 3: Iwapo shule za serikali na binafsi zingekuwa bure, ni shule ipi ungempeleka mwanao?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Asilimia 45 wanasema shule za binafsi zinatoa elimu bora ukilinganisha na shule za serikali, huku asilimia 34 wakisema kuwa shule za serikali zinatoa elimu bora. Sifa nyingine zilizotajwa kuhusu shule binafsi ni pamoja na walimu makini na wanaofanya kazi kwa bidii (asilimia 21) pamoja na uwepo wa walimu wa kutosha (asilimia 12) ukilinganisha na shule za serikali[10].

Takribani wananchi 5 kati ya 10 wanasema kuwa ubora wa elimu kwenye shule binafsi za msingi na za sekondari unaridhisha ukilinganisha na wananchi 2 kati ya 10 ambao wanasema ubora wa elimu katika shule za serikali za msingi na sekondari nao unaridhisha.

**Kielelezo cha 3a: Kiwango cha ubora wa elimu kwenye shule zilizopo kwenye eneo lako**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

10 ibid

## Jambo la 4: Wananchi wanasema wazazi kutojihusisha na masuala ya elimu ni tatizo kubwa linaloikabili sekta ya elimu

Ushahidi uliopo unaoonyesha kuwa kuna sababu mbalimbali zinazoathiri elimu na kujifunza. Chache kati ya hizo ni miundombinu duni, kushuka kwa viwango vya uandikishaji, ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na mwamko mdogo wa walimu[11]. Wananchi walipotakiwa kutaja matatizo yanayowakabili watoto ama shule wanazosoma watoto wao, zaidi ya wananchi 8 kati ya 10 (asilimia 85) wanasema kutokujihusisha kwa wazazi kwenye elimu ya watoto wao ni tatizo kubwa sana. Changamoto zingine zilikuwa ni pamoja na miundombinu ya shule (asilimia 83) na matokeo mabaya ya wanafunzi (asilimia 83).


**Kielelezo cha 4: Je, unadhani matatizo yafuatayo yanayozikabili shule ni makubwa?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Kutokujihusisha kwa wazazi/walezi kwenye elimu ya watoto wao kunajidhihirisha pale ambapo asilimia 20 ya wazazi/walezi hajawahi kuonana na mwalimu wa mtoto/watoto wao. Asilimia 57 wanawatembelea watoto wao mara moja au mara mbili tu katika kipindi cha miezi 12.

**Kielelezo cha 4a: Katika mwaka uliopita, ni mara ngapi umefanya yafuatayo:**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)


11 UNESCO-IBE (2006). *United Republic of Tanzania - Principles and general objectives of Education.* World Data on Education. 6th Edition 2006/2007. Web

Asilimia 88 ya wazazi/walezi hawajawahi kutoa msaada wowote shuleni kwa mtoto/watoto wao katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Asilimia 88 wanakubali kuwa ni jukumu lao kama wananchi kushiriki kikamilifu katika kuboresha elimu kwenye shule za serikali[12].

## Jambo la 5: Wazazi 7 kati ya 10 wanajiamini katika kushughulikia changamoto zisizo za kitaaluma zinazowaathiri watoto wao

Wananchi walipoulizwa kuhusu matatizo ya kisaikolojia yanayowaathiri watoto wa shule, asilimia 16 walitaja vishawishi vya makundi rika na umaskini kwenye kaya (asilimia 14). Matatizo ya mimba za utotoni (asilimia 12), ukatili (asilimia 5) na ajira za utotoni (asilimia 6) nayo yalitajwa.

**Kielelezo cha 5: Ni changamoto gani tatu zisizo za kitaaluma zinazowakabili watoto wa shule?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Walipoulizwa kuhusu uwezo wao wa kukabiliana na changamoto hizo, wazazi/walezi 7 kati ya 10 (asilimia 70), walisema kuwa wanaamini wanao Uwezo wa kuwasaidia watoto wao kukabiliana na changamoto hizo.

## Jambo la 6: Zaidi ya wananchi 7 kati ya 10 wanataka wasichana waendelee na shule iwapo watapata ujauzito


Kwa mujibu wa ripoti ya UNFPA kuhusu mimba za utotoni, utafiti uliofanyika kwa wanawake wenye miaka kati ya 20-24 nchini Tanzania unaonyesha kuwa asilimia 28 yao walijifungua kabla ya umri wa miaka 18[13]. Matokeo yake ni kuwa idadi kubwa ya wasichana waliacha shule kutokana na tatizo hili. Hatahivyo, Tanzania haina sera inayowaruhusu wasichana

12 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 10 (Agosti 2016). Takwimu zinapatikana: www.twaweza.org/sauti

13 Loaiza, Adilberto and Liang, Mengjia. "Adolescent Pregnancy, A review of the Evidence" *UNFPA,* 2013. Web

wanaopata mimba kurudi shuleni. Wananchi walipoulizwa kuhusu suala la wasichana kupata ujauzito wakiwa shule, asilimia 21 ya wananchi walisema kuwa wanafahamu familia ambayo mwanafunzi aliyeacha shule ya msingi au sekondari kutokana na ujauzito. Miongoni mwa wale wanaofahamu wanafunzi kama hawa, asilimia 72 wanasema wanafunzi hao walibaki kuwa mama wa nyumbani[14]. Walipoulizwa mtazamo wao juu ya hili, wananchi 6 kati ya 10 (asilimia 62) walijibu kuwa wangependa wanafunzi hao waruhusiwe kurudi shule baada ya kujifungua na asilimia 21 walisema waondolewe shuleni moja kwa moja.

**Kielelzo cha 6: Je, nini kifanyike kwa msichana anayepata ujauzito akiwa bado shule?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

## 3. Hitimisho

Kwa ujumla, muhtasari huu unaonyesha kile ambacho wananchi wanafikiri kuhusu utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo ya ada ambayo ndiyo agenda kuu ya elimu ya serikali mpya. Wananchi wengi wanaonekana kufurahishwa na juhudi zinazoendelea za kuboresha utoaji wa elimu kupitia sera ya elimu bila malipo ya ada. Hata hivyo, asilimia 60 wangependa watoto wao wasome katika shule za binafsi, japokuwa asilimia kubwa ya wananchi (asilimia 90) wanasema kuwa watoto wao wanasoma shule za serikali. Hii inatokana na imani kwamba shule binafsi hutoa elimu bora zaidi.

Sera ya elimu bila malipo ya ada inaonekana kuongeza viwango vya uandikishaji wa wanafunzi kwa kiwango cha juu. Hii ni kwa sababu vikwazo vyote vya uandikishaji vimeondolewa. Lakini je, ni kwa kiasi gani mfumo wa elimu nchini Tanzania umejipanga kuwezesha ongezeko la wanafunzi kwenye shule za serikali kujifunza na kupata stadi tarajiwa? Kinachoonekana hapa ni mvutano kati ya upatikanaji wa elimu kwa wengi, dhidi ya kuhakikisha ubora wa elimu.

14 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 10 (Agosti 2016). Takwimu zinapatikana: www.twaweza.org/sauti

Utekelezaji wa Elimu kwa Wote (UPE) ulianza mwaka 2002 nchini Tanzania. Kupitia UPE tunatambua ya kwamba kuandikisha watoto wengi shuleni kuna faida endapo tu kutakuwa na miundombinu ya kutosha na walimu pamoja na vifaa stahiki ili kuhakikisha watoto wanajifunza. Kwa namna ambavyo serikali inavyoendelea kutoa kipaumbele katika utoaji wa huduma kwa wananchi, maswali haya ya msingi hayana budi kufanyiwa kazi. Bila mikakati madhubuti tutakuwa tunaweka rehani matunda mazuri ya sera ya elimu kwa miaka ya usoni.

Wazazi ni wadau muhimu kwenye elimu japokuwa wanaonekana kujitenga na majukumu yote yanayohusiana na elimu huku wakiwa wanatambua fika kuwa wanapaswa kuhusika kikamilifu. Wananchi wengi wanasema serikali iwaondolee gharama zinazohusiana na elimu ya watoto wao. Hii inafafanua vema kwanini sera hii ya elimu bila malipo ya ada na kuondoa michango ya wazazi imekuwa maarufu sana nchini Tanzania.

Kwa kuongezea, wazazi wanapaswa kujihusisha kwa karibu na elimu ya watoto wao. Kama uhusiano baina ya wazazi na shule utaendelea kuwa duni, ni dhahiri kuwa matarajio yote ya kuboresha matokeo ya ujifunzaji yatapotea. Wazazi wana jukumu kubwa la kuwatia moyo na kuwawezesha watoto wao kufanikiwa, kwa kufuatilia utekelezaji wa sera za serikali na kuwawajibisha walimu na uongozi wa shule.


Suala moja muhimu ambalo limejitokeza kwenye muhtasari huu ni hatma ya elimu kwa wasichana wanaopata ujauzito. Kwa miaka mingi, kumekuwa na mijadala mizito kuhusu hali ya watoto wa kike wanaopata ujauzito wakiwa shule. Sera rasmi ya elimu inaelekeza wanafunzi kupimwa ujauzito shuleni na kuondolewa kwa wasichana wanaopatikana na ujauzito kwenye shule za msingi na sekondari. Kumekuwa na kampeni nyingi zinazopinga sera hii kwa madai kuwa kuwafukuza wasichana hao shuleni ni kuwaadhibu mara mbili Takwimu za muhtasari huu, hata hivyo, zinaonyesha vinginevyo. Pengine hii inaweza sasa kuishawishi serikali kufikiria upya maamuzi yake kuhusu suala hili hasa kutokana na dhamira yake ya kuboresha elimu kwa watoto wa kike. Suala hili ni muhimu likaangaliwa hususani katika kipindi hiki ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaoacha shule. Ripoti ya tathmini ya Uwezo ya mwaka 2014 inaonyesha kuwa kiwango cha kukatisha masomo kwa wanafunzi ni asilimia 18.

Kwa ujumla, Watanzania wengi wanafahamu jitihada za serikali zinazoendelea katika kuboresha utoaji wa elimu. Tathmini ya wananchi kuhusu matokeo ya elimu bado imejikita katika kuangalia vifaa vya shule na miundombinu badala ya matokeo ya ujifunzaji. Ni dhahiri kuwa mwitikio wa serikali katika kutatua changamoto za elimu unaonekana kujikita kwenye kuhimiza uandikishaji na miundombinukuliko kuainisha njia ambazo zingeweza kuboresha utoaji wa elimu, kama vile umahiri wa walimu. Matokeo yake tunabaki na janga la ujifunzaji, ambalo limedumu kwa miongo kadhaa iliyopita na linaendelea bila kufanyiwa kazi.

# Wahojiwa


Vielelezo hapo chini vinaonyesha sifa za wahojiwa wa sampuli ya *Sauti za Wananchi* kwa kulinganisha na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012. Kwa ujumla sampuli ya *Sauti za Wananchi* inaendana na idadi ya jumla ya watu nchini Tanzania.

**Kielelezo cha 7: Jinsia**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Awali wa *Sauti za Wananchi,* 2015 na Sensa ya Watu na Makazi Tanzania, 2012

**Kielelezo cha 8: Eneo la kijiografia**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Awali wa *Sauti za Wananchi*, 2015 na Sensa ya Watu na Makazi Tanzania, 2012

**Kielelezo cha 9: Umri**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Awali wa *Sauti za Wananchi*, 2015 na Sensa ya Watu na Makazi Tanzania, 2012

**Kielelezo cha 10: Elimu**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Awali wa *Sauti za Wananchi*, 2015 na Sensa ya Watu na Makazi Tanzania, 2012